# USIJE UKAJUTA

*Akasema (Huyu Mtume): "Mola Wangu! Ninusuru*
*kwa sababu wamenikadhibisha"*
*Akasema (Mwenyezi Mungu): Baada ya muda*
*Mdogo (tu hivi) watakuwa wenye kujuta."*

**HARUN YAHYA**
**(ADNAN OKTAR)**

**Kimetafsiriwa na**
**Ramadhan Rajab**
Ramadhan786@gmail.com

Kimehaririwa na
**Suleiman Chitala**
lchitala@yahoo.com

**Agosti, 2011**
**Nairobi.**

## Yaliyomo

**Utangulizi……………………..**

**Majuto Anayohisi Binadamu duniani…………………….**

**Mwanzo wa kujuta kwa makafiri ni Kifo………………..**

**Majuto Siku ya Kiyama.......................................**

**Majuto kwenye Jahannam...............................**

**Nini la kufanya usijute Siku ya Kiyama………………**

# Utangulizi

Wakati fulani binadamu akiwa duniani huwa na huzuni wa kimwili na wa kiroho. Hisia zingine ni kubwa zaidi na haziwezi kulinganishwa na uchungu wa kimwili. Hizi hisia ambazo zinailetea roho ya binadamu machungu na dhiki zinaitwa majuto.

Kuna aina mbili za majuto. Majuto ya watu wenye imani kwa upande mmoja na wasio kuwa na imani kwa upande mwingine. Hisia hizi mbili zinatofautiana sana

Waumini ni wale walio na imani thabiti kwamba lolote linalotokea ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na lolote linalowapata ni kwa kutaka kwake Mola. Ndio maana utaona waumini wana imani kwa Mwenyezi Mungu, imani ambayo haitingishiki wakati wowote uwe wa raha, au wa shida au wakifanya makosa. Mtume Muhammad (s.a.a.s) katika hadithi yake tukufu amesifu tabia ya muumini akisema:

*Mfano wa muumini ni kama mmea shambani ambao unatikiswa na upepo lakini utarudi kwa nafasi yake ambayo ni thabiti katika mizizi yake. (Muslim)*

Muumini anapotenda kosa, yeye humrudia na kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha. Kwa hivyo haumii kwa muda mrefu akisikitika. Majuto anayokuwa nayo muumini yanamsukuma aombe msamaha na kujitakasa na yanamfanya asilirudie kosa lile. Hili huwasaidia kurekebisha makosa yao na ili wasikose matumaini katika maisha. Na pia majuto haya hayapunguzi bidii yao katika mambo ya ibada.

Kwa upande mwingine, majuto ya kafiri ni ya kudumu na kuumiza kwani hawana imani na Mwenyezi Mungu pindi wanapokumbwa na shida au wakitenda kosa. Kwa maisha yao yote wao hunena “Laiti singelifanya hili…” “ Laiti singesema hivi…” na kadhalika.

Lakini watakuwa na majuto makubwa siku ya kiyama. Wale ambao hawakuishi maisha ya kidini watajuta sana. Walionywa na kualikwa kwa njia iliyonyooka. Walikuwa na wakati muafaka wa kutafakari na kufuata njia ya ukweli. Lakini hawakusikiza.

**Hakika Tunakuhadharisheni adhabu iliyo karibu (kufika), siku ambayo mtu atayaona yaliyotangulizwa na mikono yake miwili, na kafiri atasema: “Laiti ningalikuwa udongo (nisipate adhabu hii inayoningoja sasa)” (Surat an-Naba': 40)**

**Na ungeliona watakaposimamishwa motoni waseme: Laiti tungerudishwa (duniani) wala hatutakadhibisha ishara za Mola wetu na tutakuwa miongoni katika wanaoamini. (Surat al-An'am: 27)**

**“ Na watasema: “Kama tungalisikia au tungalikuwa na akili hatungekuwa katika watu wa motoni (leo) (Surat al-Mulk: 10)**

Lengo la kitabu hiki ni kuwaonya watu kwa siku ambayo watajuta wakisema” Laiti tungefahamu...,” “Laiti hatungekadhibisha aya za Mola wetu...,” “Laiti tungeliwafuata wale waliotuletea ujumbe...,” “Laiti tungelifanya hili au lile” n.k lengo pia ni kuwaita watu waishi maisha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama wangali hai ili warekebishe makosa yao.

Ni lazima kufahamu vyema kwamba majuto siku hiyo hayatamkinga mtu yeyote na hasira ya Mwenyezi Mungu. Njia pekee ya kuepukana na majuto hayo ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kama wakati bado upo na kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Kitabu hiki ni cha kulingania kwa njia ya Allah na kukumbusha adhabu isiyoepukika katika maisha ya akhera siku ambayo hakuna pa kujificha wala kuokolewa. Mwenyezi Mungu anatukumbusha kenye Qurani tukufu akisema:

**Mwitikieni Mola wenu kabla ya kufika siku isiyoepukika itokayo kwa Mwenyezi Mungu, siku hiyo hamtakuwa na pa kukimbilia wala hamtakuwa na (njia) ya kukataa. (Surat ash-Shura: 47)**

# Majuto Anayohisi Binadamu duniani

**Na rejeeni kwa Mola wenu na mnyenyekee kwake kabla ya kukujieni adhabu, kisha hamtanusuriwa. Na fuateni yaliyo bora katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu kabla kukujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui. (Surat az-Zumar: 54-55)**

Binadamu akiwa katika hatari ya mauti, nafsi yake inaanza kufanya hesabu ya matendo yake. Kama mtu hakuishi katika maadili ya kidini ya Mwenyezi Mungu na wala hakufanya matendo mazuri duniani, basi atakumbwa na huzuni na majuto makubwa. Mambo mengi ambayo alidharau kwa maisha yake yote yatajitokeza mbele ya macho yake kwa uwazi. Labda kwa mara ya kwanza atahisi vipi mauti yako karibu sana. Atakiri kwamba aliishi maisha ambayo hastahiki kupata pepo. Binadamu huyo atajua kwamba alikosa shukrani kwa Mwenyezi Mungu. Hofu kubwa itamzunguka na atajua kwamba ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye atamuokoa kwa hali ambayo yuko. Kisha atamuahidi Mwenyezi Mungu kuwa atakuwa na shukrani na kufuata njia ya haki na kukumbuka hali ambayo yuko. Anamuomba Allah kwa dhati amuokoe kwa hatari ambayo yumo. Anaomba nafasi ya kuokolewa na kuomba fursa ya kuishi tena.

Lakini baada ya kuokolewa na mauti, binadamu wengine hawaweki ahadi ambayo walimuahidi Mwenyezi Mungu. Pindi Mwenyezi Mungu Anamuokoa mtu huyo, anarudi kwa njia zake za awali. Hisia za majuto na kusalimu zinabadilishwa na ukosefu wa shukrani. Anasahau yale alifikiria wakati alikumbwa na mauti na anamsahau Mwenyezi Mungu kana kwamba hakujuta na kumuomba. Anarudia matendo yake na kuipenda dunia zaidi. Qurani tukufu inaashiria hisia za watu kama hawa:

**Yeye ndiye anayekuendesheni katika bara na bahari. Hata mtakapokuwa katika majahazi Na yanakwenda nao Kwa upepo mzuri Na wanafurahi nao; mara upepo mkali unayajia Na mawimbi yanawajia kutoka kila upande, na wanaanza kufikiri ya kwamba wametingwa. (hapo ndipo) wanapomuomba mwenyezi Mungu kwa kumtakasia utii, wakisema: "Ukituokoa katika haya bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru."**

**Lakini anapowaokoa, mara wanafanya maasi (tena) katika ardhi bila haki. "Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Na starehe (chache tu) za maisha ya dunia, kasha marejeo yenu yatakuwa kwetu. Hapo tutakuambieni (yote) mliyokuwa mkifanya." (Surah Yunus: 22-23)**

**Na inapokufikieni taabu katika bahari, hupotea wale mnaowaita isipokuwa Yeye tu. Lakini anapokufikisheni salama nchi kavu, mnakengeuka. Ama mwanadamu ni mwingi wa kukanusha. Je! Mmesalimika kuwa hatakudidimizeni upande wa nchi kavu au kuwaletea tufani la kokoto, kisha msipate wa kutegemea? (Surat al-Isra: 67-68)**

Kama vile imesisitizwa kwenye aya hii, vipi mtu atakuwa na uhakika kwamba hatakumbwa na shida kama hiyo au zaidi

ya hiyo kwa mara nyingine. Na pia vipi mtu atakuwa na uhakika kuwa ataokolewa tena. Bila shaka hakuna aliye na uhakika kuwa mambo haya hayawezi kutendeka. Kwani mwishowe kila mtu atakufa wakati wake ukifika. Na majuto hayatakuwa na manufaa yoyote.

Na hii ndio hali inayowakumba wale ambao hawaambatanishi maisha yao na dini. Mwenyezi Mungu Anaeleza hali hii kama ifuatavyo:

**Na dhara inapomgusa mtu hutuomba (anapolala) ubavu, au hali ya kukaa au kusimama. Lakini tunapomuondolea dhara yake hupita (akafanya yake atakayo) kama kwamba hakutuomba tumuondeshee dhara iliyompata. Namna hivi wamepambiwa wapitao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda. (Surah Yunus: 12)**

**Yakiwapata watu madhara humuomba Mola wao kwa kumnyenyekea, kisha Anapowaonjesha rehema Yake, hapo baadhi yao mara humshirikisha Mola wao. (Surat ar-Rum: 33)**

Watu waliotajwa katika aya hizi ni wale wanamrudia Mwenyezi Mungu wakiwa na matatizo. Na pindi shida zao zikiondolewa wanasahau ahadi walizoweka kwa Mwenyezi Mungu na kukosa shukrani. Hii yaonyesha kwamba majuto waliyokuwa nao ni kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kujiokoa.

Lakini kwa upande mwingine majuto ya waumini ni tofauti na vile tumetaja hapo juu kwani majuto yao ni ya manufaa. Majuto ya kweli hayasauliki haraka. Majuto hayo huwa ni ya mabadiliko makubwa pamoja na kurekebisha tabia ya mtu. Yeyote ambaye ana majuto ya kweli kwa moyo wake ataishi maisha yake yote kulingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu akitarajia rahma na msamaha wa Mwenyezi Mungu. Anapopata neema harudi kwa makosa aliyokuwemo kwa anaona huo ni ukosefu wa shukrani na itakuwa ni hasara kwake.

Mwenyezi Mungu Anaeleza hali ya kisaikolojia ya watu wanaokabiliwa na mauti wakiwa kwenye meli ili iwe onyo kwa watu wote. Hii ni kwa sababu hali hii hupatikana kwa kila binadamu. Kwa hivyo ili kunufaika na funzo lililotajwa kwenye aya zilizotajwa, ni lazima kuepukana na mambo mabaya ya kiroho na kujihesabu nafsi yake na kisha kujiuliza swali hili:

"Nafsi yangu ingekuwa kwa hali gani kwama ningekumbwa na mambo hayo.? Je nini ningelifanya ili nionyeshe kujuta? Ni mabadiliko gani ningefanya kwa tabia yangu kama nikiokolewa? Ni maasi gani ningeepukana nayo na nini ningeazimia kufanya."

Ni vizuri kutafakari kuhusu haya mambo hata kama humo hatarini kwani yaweza kuja wakati wowote na pia yawezekana kwamba hutawahi kupata hatari kwa maisha yako. Lakini ukweli ni kwamba kifo kifikapo, mtu atajikuta ghafla amezungukwa na malaika wa kifo. Na wakati huo atafahamu ukweli wa kifo na kama hakuishi kulingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa hakika, atakuwa ni mwenye kujuta.

Ili kuepukana na majuto ya hapa duniani na akhera, kitu cha pekee cha kufanya ni kumrudia Mwenyezi Mungu, kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu kama vile imenukuliwa katika Qurani. Mauti yapo karibu sana, kwa hivyo binadamu

asichelewehe kufanya mambo ambayo anafaa kuyafanya. Lazima aazimie kufanya matendo mema kwa subra na bidii. Ni lazima mtu awe na ikhlasi na kuwa karibu na Mwenyezi Mungu kama vile anavyohisi wakati akiwa kwenye shida.

Ni muhimu kukumbuka kwamba lengo la kuumbwa binadamu ni kumuabdu Mwenyezi Mungu na kuwa mja mwema atafutaye radhi ya Mwenyezi Mungu. Mambo mengine duniani kama vile mali, familia, kazi n.k ni namna ya kumfikisha mja karibu na Mwenyezi Mungu. Na wote wanaotafuta vitu hivi na kusahau kwamba wamepewa neema na Allah ili wamshukuru, watakuwa wenye kuhasirika. Manufaa ya muda yanayopatikana duniani hayatakuwa na maana siku ya akhera. Katika Qurani Mwenyezi Mungu anasema kwamba hawa ni watu watakaokuwa na huzuni kubwa.

**Sema: Je! Tukujulisheni wenye hasara katika vitendo (vyao)? Hao ambao bidii yao (hapa duniani) imepotea bure katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanafanya amali njema! Hao ni wale waliozikataa (waliozikanusha) Ishara za Mola wao na (wakakataa) kukutana naye. Kwa hivyo vitendo vyao vimeharibika, wala hatutawasimamishia mizani Siku ya Kiyama (Surat al-Kahf: 103-105)**

Mradi mtu anafikika kiwango cha kuridhiwa na Mwenyezi Mungu hapa duniani kupitia tabia njema na vitendo vyema, Mwenyezi Mungu atamlinda duniani na akhera. Lakini akipoteza fursa hii duniani, atajuta sana wakati malaika wa kifo wanapomjia. Fursa hii itakuwa vigumu kulipizwa na itakuwa ni majuta ya kudumu –isipokuwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Katika Quran Allah Anaeleza majuto siku watu watahisi wakiwa mbele yake hivi:

**Atasema: "Laiti ningalitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo)". (Surat al-Fajr: 24)**

**... na akawa anasema, "Laiti nisingalimshirikisha Mola wangu na yoyote!" (Surat al-Kahf: 42)**

**... "Laiti ningalishika njia (ya haki nikawa) pamoja na Mtume!"**

**(Surat al-Furqan: 27)**

Yeyote ambaye hangependa kunena maneno haya ni lazima achukue nafasi wakati huu ajisalimishe kwa Mwenyezi Mungu na aishi kulingana na sheria Alizoziweka Muumba wetu.

**Ni lazima kujihadhari na majuto anayohisi mtu hapa duniani**

Maisha ya duniani ni fursa nzuri aliyopewa mwanadamu ili apate maisha mema na ya kudumu ya akhera.

Wale ambao hawatumii hii fursa na wanaishi maisha yasiyoambatana na dini ya Kiislamu watajuta kuishi kwao duniani watakapoona adhabu ya akhera. Hii ni kwa sababu walionywa mara nyingi na kufahamishwa aina mbili ya makazi - Janna (Pepo) na Jahannam (moto). Na pia walifahamishwa kuwa nyenendo zao ndizo zitaamua makazi gani watachuma. Kama

vile anatufahamisha Mtume Mtukufu (s.a.a.s) : “ dunia ni shamba la akhera.” (*Ihya' al-ulum* ) .

Mwenyezi Mungu Mkarimu Anawapa binadamu mafunzo ya majuto duniani kwa kusisimua fikra na hisia zao ili wasije kufikia kiwango hiki kibaya. Na pia Mwenyezi Mungu Anawapa watu muda maalum ili wajitakase kutokana na makosa yao na tabia mbaya. Kila binadamu katika maisha yake, anapewa fursa ya kutubu na kuishi maisha yaliyobaki kwa njia ya Mwenyezi Mungu.

Ukizingatia haya utaona kwamba hisia ya majuto ni fursa kubwa ambayo Mwenyezi Mungu amempa binadamu. Hii ni kwa sababu yeyote anayejuta kwa moyo wake wote na kumrudia Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humpa uongofu wa kudumu kwa ikhalsi yake. Kinyume cha hayo, yeyote anepuuza onyo na fursa hii, basi adhabu yake itakuwa kubwa na hataokolewa kutokana na huzuni isipokuwa kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Katika Qurani, Mwenyezi Mungu Anatuonyesha mifano ya watu waliojuta makosa yao. Hizi hisia za majuto ziliwapelekea kikundi cha watu kumrudia Allah na Akawaokoa

**Bila Shaka Mwenyezi Mungu Amekwisha pokea toba ya Mtume na Muhajiri na Ansari waliomfuata yeye (Mtume ) katika ile saa ya dhiki; wakati ambao nyoyo za kundi moja miongoni mwao zilikuwa karibu kugeuka (kufuata ukafiri); basi akawaelekea (Mwenyezi Mungu) kwa rehema. Kwa yakini yeye (Mwenyezi Mungu) kwao ni Mpole (na) Mwenye rehema.**

**Na (pia akawaelekea kwa rehema) wale watatu walioachwa nyuma (kukubaliwa toba yao kwa yale makosa yao makubwa waliyoyafanya); hata ardhi ikawa finyu juu yao, pamoja na wasaa wake; na nafsi zao zikadhikika juu yao, na wakayakinisha ya kwamba hapana pa kumkimbilia Mwenye Mungu ila (kuelekea) Kwake, kisha (Mwenyezi Mungu) akawaelekea ili wapate kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye apokeaye toba na Mwenye rehema. . (Surat at-Tawba: 117-118)**

Kama vile tunafahamu kutokana na aya hizi, watu watatu walioachwa nyuma, walipata majuto makubwa kwenye nyoyo zao. Na kwa hivyo walitambua kuwa njia pekee ya kujiokoa ni kuomba msamaha na kumrudia Mwenyezi Mungu. Ni majuto haya ya ukweli ambayo huwahamasisha na kuwabadilisha watu na pia kuwafanya warekebishe makosa yao. Watu aina hii wataishi maisha ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu rehema Zake. Mwenyezi Mungu Anatufahamisha katika Qurani kwamba kwa hakika anakubali msamaha kutoka kwa waja wake na kuwasamehe:

**Ila Yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri; basi hao ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.**
**Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatubu kwa Mwenyezi Mungu toba ya kweli. (Surat al-Furqan: 70-71)**

**Na wale waliotenda maovu, kisha wakatubiya baada yake na wakaamini, hakika Mola wako baada ya hayo ni mwenye kusamehe mwenye kurehemu (Surat al-Araf: 153)**

**Na hakika Mimi ni Mwenye kusamehe sana kwa anayetubia na kuamini na kutenda mema, tena akashika uwongofu. (Surah Ta Ha: 82)**

Vile vile imesimuliwa katika Qurani kwamba watu ambao walitumiliwa na mitume walijuta matendo yao maovu. Kama vile watu wa Nabi Musa (as) ambao hawakuweza kumsubiri arejee kutoka mlima Sinai na wakamsahau Mwenyezi Mungu na wakarudia kuabudu sanamu. Mwenyezi Mungu anaonyesha toba kubwa walioifanya watu hawa kwa madhambi yao:

**Na baada yake watu wa Musa walimfanya katika mapambo yao kiwiliwili cha ndama kilichokuwa na sauti. Je, hawakuona kwamba huyo hasemi nao wala hawaongozi njia? Walimfanya (mungu) na wakawa wenye kudhulumu.**

**Na walipojuta na wakaona kwamba wamekwishapotea walisema: Kama Mola wetu hatatuhemu na kutusamehe bila shaka tutakuwa miongoni mwa waliopata hasara (Surat al-A'raf: 148-149**

Mwenyezi Mungu anasisitiza tena kwenye Qurani kuhusu hadithi ya wenye shamba. Mwenyezi Mungu aliwapa shamba kama neema. Lakini walikuwa wajeuri na wakaona shamba kama ni lao, na wakasahau kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo adhabu waliyoipata iliwafanya wajute vitendo vyao na kumrudia Mwenyezi Mungu. Aya zinazoeleza kuhusu wenye shamba ni kama ifuatavyo:

**Hakika tutawatia kwenye mtihani (Makureshi) kama tulivyowatia mtihanini wenye shamba, walipoapa kwamba watayavuna (mazao yake) itakapokuwa asubuhi (ili wasionekane na maskini wakaombwa). Wala hawakusema: Inshallah. Basi ulilifikia (shamba hilo) msiba mkubwa utokao kwa Mola wako; na hali wao walikuwa wamelala. Ikawa kama iliyong'olewa. Asubuhi wakaitana ya kwamba: "Nendeni mapema kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna. Basi walikwenda na huku wakinong'onezana ya kuwa: Leo maskini asiingie humo mwenu" na wakenda asubuhi, hali wanadhani kuwa wanao uwezo wa kuzuia. Basi walipoona wakasema: "Bila shaka tumepotea. Bali tumenyimwa. Mbora wao akasema: "Je! Sikukuambieni, (msitie nia mbaya ya kuwazuilia haki yao maskini? Sasa) rejeeni kwa Mola wenu, mtubie kwake." Wakasema: "Utukufu ni wa Mola wetu! Hakika tulikuwa madhalimu. Basi wakakabiliana kulaumiana. Wakasema: "Hasara yetu! Hakika tulikuwa tumeruka mipaka (ya Mwenyezi Mungu) huenda Mola wetu Atatubadilishia (shamba) lililobora kuliko hili; hakika sisi tunajipendekeza kwa Mola wetu" (Surat al-Qalam: 17-32)**

Lakini hali zikibadilika au watu wakipewa fursa, wengi wao husahau onyo ambalo lengo ni kuwafanya wajute, watubie, na kuwafanya watende mambo mema. Wale ambao wanapuuza onyo na kurudia nyendo zao kwa kweli wataadhibiwa ikiwa hawatatubia kwa wakati kama vile ilitendeka na watu wa Thamud, watu wa Nabi Salih (a.s). Watu hawa walikataa onyo ya Nabi Salih (a.s) mbali na kujua kwamba watajuta kuangamizwa kwao. Kwa hakika Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake ya kutekeleza amri Yake. Mwenyezi Mungu Anatujulisha haya ili iwe funzo kwa watu wote:

**Akasema: Huyu ngamia jike; awe na zamu yake ya kunywa na nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalum. Wala msimguse kwa ubaya isije ikawashika adhabu ya siku kubwa. Lakini wakamuua wakawa wenye kujuta. Basi ikawashika adhabu. Hakika bila shaka katika hayo ipo ishara, lakini wengi wao si wa kuamini.**

**Na hakika Mola wako ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu. (Surat ash-Shu'ara: 155-159)**

Ni lazima tukumbuke kwamba Mwenyezi Mungu ni Muadilifu na haachi kosa lolote bila kulipiza lakini kwa upande mwingine analipa watu kwa matendo mazuri waliofanya kwa ajili yake. Anawapa habari njema ya rehema na pepo kwa wale wanaomuelekea na kutubia kikweli. Ukizingatia haya ni lazima ujiulize, je waweza kulinganisha majuto ya hapa duniani na majuto ya akhera ambayo ni ya milele? Bila kusahau kwamba majuto ya akhera yatakuwa kwenye jahanam.

Kwa hakika hakuna mtu ambaye angependa kufikia kiwango cha kujuta siku hiyo ya kiyama. Kwa hivyo ni lazima kila mtu atumie fursa aliyonayo akiwa bado duniani. Yeyote anayetumia neema hii ya Mwenyezi Mungu si tu ataokolewa na moto bali pia atapata baraka za hapa duniani na akhera.

Kwa hivyo yeyote ambaye anafanya bidii ya kupata hizi baraka na kuepuka majuto ya watu wa motoni ni lazima ajitakase kwa kumridhisha Mwenyezi Mungu. Na ni lazima afuate ile njia ya kumtoa kutoka kwa giza hadi kwenye nuru (mwangaza) Mwenyezi Mungu anatuelezea katika aya hizi:

**Yeye ndiye anayewaswalia na malaika wake, ili awatoe katika giza na kuwatia katika nuru. Naye ni mwenye kuwarehemu waumini. Maamkuzi yao siku ya kukutana naye yatakuwa ni Salaam na amewaandalia malipo yenye heshima. (Surat al-Ahzab: 43-44)**

# Mwanzo wa kujuta kwa makafiri ni Kifo

## Kila nafsi itaonja mauti, na tunakufanyieni mitihani kwa shari na ya kheri; na kwetu (nyote) mtarejeshwa.

**(Surat al-Anbiya': 35)**

Wale ambao hawaamiini akhera wanachukulia mauti kama ndio mwisho wa kila kitu. Hii ni fikra potofu kwani kifo sio mwisho bali ni mwanzo. Kwa waumini ni mwanzo wa maisha mazuri, pepo ya kudumu ambayo haina maovu wala upungufu.Na kwa makafiri ni safari ya kuelekea motoni pahali palipo na adhabu kali.

Wale ambao wanafahamu ukweli huu hupata raha wakati mauti yanapowafikia na kisha maisha ya raha akhera.

Lakini kwa upande mwingine, makafiri watajuta wakifikiwa na mauti na watakumbuka yale waliyoonywa. Watapata adhabu na hawatakuwa na hiari ya kukimbia kwa kadiri Mwenyezi Mungu atapenda.

Hata kama binadamu hapendi kutafakari kuhusu mauti, ni kitu cha lazima. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ameumba kifo kama mwisho wa maisha ya duniani. Hadi leo, hakuna mtu yeyote ambaye ameweza kuepuka kifo. Hakuna cha kuokoa mtu yeyote na kifo, iwe mali, kazi au marafiki wandani. Kwa hakika kila mtu lazima akumbane na mauti. Mwenyezi Mungu aeleza hili katika aya nyingi za Qurani:

**Popote mlipo mauti yatakufikieni, hata mkingiwa katika ngome madhubuti . (Surat an-Nisa: 78)**

**Sema: Hakika mauti mnayoyakimbia, bila ya shaka yatawakuta. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye kuyajua ya ghaibu na yanayoonekana. Hapo atawaambia mliyokuwa mkiyatenda. (Surat al-Jumu'a: 8)**

**Wala Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapofika wakati yake; na Mwenyezi Mungu ana habari ya mnayotenda . (Surat al-Munafiqun: 11)**

Je! Kutotafakari kuhusu mauti na maisha baada ya kifo kutamuepusha mtu na ukweli? Kwa hakika jawabu ya swali hili ni "La". Kwa vile binadamu ni mwingi wa kuhangaika kuhusu kifo, la maana kufanya ni kutafakari kila wakati kuhusu kifo na kujiandaa kwa maisha ya akhera, kama vile Mtume Muhammad (s.a.a.s) alituelezea *"Tafakari kuhusu kifo kwa wingi. Mwenyezi Mungu hufungua moyo wa yule anayetafakari kuhusu kifo na hufanya kifo chake chepesi"* (Imeripotiwa na Abu Huraira)

Wale ambao wanapuuza kutafakari kuhusu maisha ya akhera kwa kupotezwa na mambo ya dunia watashangazwa na mauti. Wale ambao wanasema " kwa vile bado tuko kwa ujana na lazima tuutumie vizuri na baadaye ndipo tutafikiria kuhusu kifo" watajua kwamba hawatawahi kupata fursa kama hiyo. Hiyo ni kwa sababu mauti yamekadiriwa na Mwenyezi Mungu. Yawezekana mtu afariki kabla hajazeeka. Kwa hivyo kufanya mipango ya baadaye bila ya kutekeleza maamrisho yake kutapelekea mtu kwa majuto makubwa.

Wale ambao huishi maisha yao kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kutubia wakati wanapoona mauti yako karibu, watakuwa na majuto kama haya. Lakini kutubia kunakotokana na hofu ya mauti bila ya niya safi ya kujitakasa yaweza kukataliwa na Mwenyezi Mungu. Watu kama hawa waliopenda dunia kupita kiasi hutaka kuokolewa mauti yanapokaribia na hii haitowafaidi na lolote. Mwenyezi Mungu anajua niya yao mbaya kwani Yeye Mwenyezi Mungu yuko karibu na binadamu zaidi kuliko mshipa wa damu Anajua yaliyomo ndani ya binadamu pamoja na fikra zake za ndani na siri zake za ndani. Mwenyezi Mungu Anatufahamisha katika Qurani kwamba Hatakubali tauba inayotokana na hofu ya mauti kwa dakika ya mwisho.

**Na si toba ya wale ambao hufanya maovu mpaka mmoja wao akafikiwa na mauti akasema: sasa mimi nimetubia, wala ambao hufa wakiwa makafiri. Hao tumewaandalia adhabu iumizayo**

**(Surat an-Nisa: 18)**

Na imetajwa katika aya nyingi kwamba watu kama hawa ambao nia yao si safi wakipewa fursa nyingine wao hurudia nyendo zao za ukafiri.

**Na ungeliona watakaposimamishwa motoni waseme: Laiti tungerudishwa (duniani) wala hatutakadhibisha ishara za Mola wetu na tutakuwa katika wanaoamini. Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangalirudishwa, bila shaka wangeyarudia yale waliyokatazwa na hakika wao ni waongo. (Surat al-An'am: 27-28)**

Kwa hivyo ni makosa kuwa na itikadi kwamba 'nitatubia ikifika wakati mwafaka' kwani fikra kama hii haitamuokoa mtu kutokana na adhabu ya moto. Basi ikiwa mtu hataki kupata adhabu kali ya milele baada ya ya kifo, ni lazima aishi maisha yenye lengo, akijua kwamba bila shaka atakutana na Mwenyezi Mungu na atatoa hesabu ya vitendo vyake.

## Majuto ya makafiri wakati wa mauti

Watu wengi maishani mwao wamekuwa wakikumbushwa kuhusu pepo na jahanam na kwamba lazima wajitayarishe kwa maisha ya akhera. Lakini makafiri wanafunga masikio yao kwa maonyo haya. Wakati wanafikiwa na mauti, watakiri kwamba walijipelekea wenyewe kwenye uangamizi. Hakuna aliyewalazimisha, wao wenyewe kwa chaguo lao, wamefikia mwisho mbaya. Wakati wa mauti makafiri wanaanza kuumia kwa huzuni. Hofu kubwa inayowakumba mwanzo wa mauti yao ni ishara ya adhabu ambayo Mwenyezi Mungu anaielezea katika Qurani akisema:

**Na utakapoambatanishwa muundi kwa muundi. Siku hiyo ndiyo kupelekwa kwa Mola wako! Basi hakusadiki, wala hakuswali. Bali alikanusha, na akageuka. Kisha akenda kwa watu wake kwa matao. Ole wako, tena ole wako! Kisha ole wako, tena ole wako! (Surat al-Qiyama: 29-35)**

Ni lazima tujue kwamba ni makafiri ndio wanapata adhabu ya hofu hii. Waumini wanaishi maisha yao kutenda mema ili kumridhisha Mwenyezi Mungu na kupata mapenzi Yake. Kwa sababu hii kila mara wao wana matumaini. Kinyume na makafiri ambao hupata majuto makubwa wanapojiwa na mauti. Lakini kwa bahati mbaya majuto haya hayaondoshi adhabu kwani ni majuto ya kuchelewa. Katika Qurani imetaja kwamba wakati makafiri wanafikiwa na mauti roho zao hutolewa kwa uchungu na uzito.

**… Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyoshea mikono yao (na kuwaambia) "zitoeni nafsi zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu pasipo haki, na kwa vile mlivyokuwa mkizifanyia kiburi Aya Zake," (Surat al-An'am: 93)**

**Basi itakuwaje (hali yao), Malaika watakapoifisha? watawapiga nyuso zao na migongo yao. (Surah Muhammad: 27)**

Hakika ni vigumu sana kuelewa yale yanayowapata makafiri wakati wa kifo. Lakini Mwenyezi Mungu Anatuonyesha picha ili mwanadamu atafakari na kuepuka kufikiwa na jambo kama hili wakati wa mwisho. Malaika wa mauti, kama vile aya zinatueleza watatoa roho za makafiri ilihali wakiwapiga kwa nyuso zao na migongo yao. Wakati huo, watapata machungu ya kimwili ikiandamana na majuto makubwa kwani watafahamu kwamba hawatapata fursa ya kurudi duniani.

Wakati wa mauti, mwanadamu ataona wazi yale ambayo atakumbwa nayo. Huu ndio mwanzo wa maisha ya milele. Kifo ni njia ya kuvuka tu kwani ni kutolewa roho kwenye kiwiliwili.

Kulingana na adhabu wanayoipata, makafiri wanafahamu kwamba adhabu hiyo ni ya kudumu. Wale wote walioishi maisha yao bila ya kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu wanaanza kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha na amani. Wanamuomba warudishwe duniani ili wafanye matendo mema ambayo hawangeweza kufanya. Lakini matakwa yao hayatakubaliwa "**kwani walipewa maisha ya kutosha ili wapate mawaidha."** kama vile Mwenyezi Mungu Anataja kwenye aya. Walipewa bishara ya pepo na onyo kuhusu jahannam lakini waliyapa mgongo maneno ya ukweli. Mwenyezi Mungu anasema kwamba watakataa ukweli lau wakipewa fursa nyingine.

**Hata yanapomfikia mmoja wao mauti husema: "Mola wangu! Nirudishe (ulimwenguni). Ili nifanye mema sasa katika yale niliyoyaacha. (Hujibiwa na Malaika akaambiwa) "Hapana!" Hakika hili ni neno tu analolisema yeye......**

**(Surat al-Muminun: 99-100)**

Makafiri kwa makusudi walikataa kumsujudia Mwenyezi Mungu, na kukataa kufuata maamrisho Yake na pia kutokuwa na tabia nzuri. Mwenyezi Mungu Anasema katika Qurani kwamba wakati mauti yanawafikia hawawezi kamwe kumsujudia.

**Hiyo siku kutakayokuwa na mateso makali, na wataitwa kusujudu lakini hawataweza. Macho yao yatainama chini; unyonge utawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa kusujudu walipokuwa salama (na walikataa) (Surat al-Qalam: 42-43)**

Nukta nyingine ya kuongezea ni kwamba makafiri wanapojuta wakati wa mauti wanafahamu kwamba ahadi za Mwenyezi Mungu ni za kweli. Kwa upande mwingine waumini ambao hawakuaminiwa na makafiri na pia kufanyiwa masikhara wakiwa duniani, hawapati huzuni wanayoipata makafiri siku kama hiyo. Waumini wanalipwa malipo mema kwa sababu umri wao wote waliishi wakitaka radhi za Mwenyezi Mungu. Kinyume na makafiri, roho za waumini zinatolewa kwa upole bila uchungu. (Surat an-Naziat: 2). Kama vile Mwenyezi Mungu Anataja kwenye aya, Malaika wanawasalimia waumini na kuwapa bishara ya pepo.

**Wale ambao Malaika huwafisha katika hali njema, wakasema: "Amani iwe juu yenu; ingieni Peponi kwa sababu ya yale (mema) mliyokuwa mkiyatenda. (Surat an-Nahl: 32)**

Na hii ni adhabu ya kisaikolojia kwa makafiri. Walipewa fursa sawa ambayo walipewa waumini duniani. Lakini wao waliuza akhera ya pepo kwa maisha mafupi ya dunia. Licha ya kukumbushwa kwamba dunia ni pahali pa mtihani kwa mwanadamu na kwamba maskani ya kweli ni akhera, wao walijifanya kutojua. Kwa hivyo hawakufanya matendo ya

kustahikia pepo. Makafiri wanapoona mazuri wanaopata waumini, majuto yao huongezeka.

Mwenyezi Mungu asema katika aya moja:

**Je! Wanafikiri wale waliofanya maovu kuwa tutawafanya kama wale walioamini na kutenda mema kwamba maisha yao na mauti yao yawe sawa? Ni mabaya wanayoyahukumu. (Surat al-Jathiyya: 21)**

Kwa hivyo kila mtu atalipwa vilivyo, wema na bishara na waovu kwa adhabu kali.

Hofu itawajaa makafiri zaidi wakijua kuwa wametayarishiwa Jahannam baada ya kuonja uchungu wa mauti. Hakika huo uchungu unawaashiria adhabu inayofuatia.

Majuto haya ya makafiri ambayo yanaanza na mauti yatadumu kama vile atataka Mwenyezi Mungu, watabaki kwenye adhabu ya kudumu na hawataokolewa na kujuta.

Lakini kila binadamu anaweza kuepuka adhabu ya majuto makubwa. Kungoja wakati wa mauti si njia peke yake ya kuweza kujua uhakika wa mauti na maisha ya baadaye. Kwa waumini, ahadi ya Mwenyezi Mungu inatosha. Baada ya kifo, uadilifu wa Mwenyezi Mungu ndio utabaki; makafiri wataadhibiwa kwa moto nao waumini watalipwa kwa pepo.

Kwa hivyo jambo la hekima analopaswa kufanya mtu kabla hajafikiwa na mauti ni kuomba kinga kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kumuomba msamaha wake. Na pia lazima mtu azingatie Qurani ambayo ndio njia pekee ya kuongoza wanadamu kwa njia iliyonyooka na pia kuelewa na kufuata sunnah ya Mtume Mtukufu (s.a.a.s). Badala ya kuhepa kutafakari kuhusu mauti, mtu atapata faida ikiwa atafikiria kuhusu mauti na kutenda mema.

Yule ambaye anamuelekea Mwenyezi Mungu atapata radhi katika dunia na akhera na ataingia pepo, akiwa ameridhia

**Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayopata) na (Mwenyezi Mungu) aridhike nawe. Basi ingia katika (kundi la) waja Wangu (wazuri) Uingie katika Pepo Yangu. (Surat al-Fajr: 27-30)**

Njia ya kuokolewa na majuto na kupata maisha mazuri ya akhera ni kutafakari kuhusu mauti na akhera na kufuata njia ya

Mwenyezi Mungu, Muumba wa binadamu.

# Majuto Siku ya Kiyama

**Na litapigwa baragumu watazimia waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila Yule amtakaye Mwenyezi Mungu. Tena litapigwa mara nyingine, ndipo watasimama wakiangalia. Na ardhi (siku hiyo) itang'aa kwa nuru ya Mola wake, na daftari (ya vitendo) itawekwa; na wataletwa Manabii na mashahidi, na kutahukumiwa baina yao kwa haki wala hawatadhulumiwa. Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyoyafanya, naye (Mwenyezi Mungu) anajua sana wanayotenda. (Surat az-Zumar: 68-70)**

Wote ambao waliishi duniani watafufuliwa siku ya kiyama. Wakati wa kufufuliwa ni wakati mgumu kwa makafiri.

Mwenyezi Mungu katika Qurani Anataja hofu na mazungumzo ya kushangaa baina ya makafiri wakati wa kufufuliwa

**Wanasema, "Ole wetu! Nani aliyetufufua malaloni petu?" "Haya ndiyo yale anayoahidi (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema na waliyoyasema kwa haki Mitume." (Surah Ya Sin: 52)**

**Na itafika ile ahadi ya haki. Hapo ndipo yatakodoka macho ya wale waliokufuru (wakisema): "Ole wetu! Bila shaka tulikuwa katika mughafala na (Jambo) hili, bali tulikuwa madhalimu (wa nafsi zetu) (Surat al-Anbiya': 97)**

Matumizi ya maneno "Ole wetu" yanaashiria hofu kubwa na kutetemeka kwa makafiri. Wakati wa kufufuliwa, watajua kwamba wale waliowaonya kuhusu akhera walikuwa wakweli. Kwa masikitiko makubwa, wanafahamu sasa kwamba onyo hizo zitaonekana moja baada ya nyengine. Wakati huu wote hawatakuwa na njia ya kutoroka wataingizwa kwa adhabu ambayo hawakudhania mbeleni kama ni ukweli

Baada ya kufufuliwa, makafiri watasimamishwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Kisha watahitajika kutoa hesabu ya yale waliyofanya duniani na kisha uamuzi utafanywa vilivyo. Kwa sababu hii, wataletwa mbele ya Mwenyezi Mungu pamoja na wenye kiburi wale ambao walipitisha mipaka alizoweka Mwenyezi Mungu.

**Siku itakapopigwa parapanda nanyi mtafika makundi makundi (Surat an-Naba: 18)**

Kaitika hiyo siku ya kiyama, makafiri watafahamu kwamba hakuna jambo la muhimu isipokuwa kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kuepukana na hasira Zake. Hili pia limetajwa kwenye hadithi ya Mtume Mtukufu (s.a.a.s) ambapo alitoa mfano wa kafiri anapoulizwa siku ya kiyama:

*Kafiri ataletwa Siku ya Kufufuliwa na ataulizwa. " Je! Lau ungekuwa na dhahabu kiasi cha dunia nzima, je ungetoa kuokoa nafsi yako? Atajibu: "Naam" Kisha ataambiwa, " Uliulizwa ufanye jambo lepesi kuliko hilo (maana kuukubali Uislamu, lakini ulikataa)*

Majuto yao yanaongezeka kwa kuwa hawakuzingatia ishara za uwezo wa Mwenyezi Mungu na kuwepo kwake zilikuwa dhahiri. Siku hiyo wataona kwa uwazi kwamba walipoteza fursa hii. Majuto yao yataonekana namna wanazungumza.

**Na siku (hiyo) dhalimu atajiuma mikono yale na huku akisema : "Laiti ningalishika njia (ya haki nikawa) pamoja na Mtume!" Ee ole wangu! Laiti nisingalimfanya fulani rafiki. Amenipoteza nikaacha mawaidha baada ya kunijia;" na kweli shetani anamtupa binadamu. (Surat al-Furqan: 27-29)**

Siku ya kiyama, makafiri watajishughulisha na shida zao mpaka watasahau mwito wa watoto wao, wake zao, mama zao na baba zao. Tunafahamishwa kwenye Qurani kwamba:

**Basi itakapokuja sauti kali iumizayo mashikio. Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye, na mamaye na babaye, na mkewe na wanawe. Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na hali itakayomtosha mwenye, (hana haja ya mwenziwe) (Surah Abasa: 33-37)**

Fikra ya nasaba au familia inakosa maana. Toka hapo kitu ambacho anatafuta ni kuokolewa na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa hili ndilo muhimu siku hiyo, makafiri watakuwa radhi kutoa fidia watoto wao wenyewe, wake zao, ndugu zao n.k

**Siku mbingu zitakapokuwa kama shaba iliyoyayuka. Na milima itakuwa kama sufi. Wala jamaa hatamuuliza jamaa (yake). Watafanya waonane. Mwenye kosa atatamani ajikomboe katika adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa watoto wake. Na mke wake na ndugu yake. Na jamaa zake waliomzunguka kwa kila upande. Na (kuvitoa) vyote vilivyomo katika ardhi, kisha aokoke. . (Surat al-Ma'arij: 8-14)**

Kwa hakika juhudi hizi za makafiri zitaambulia pa tupu. Lengo kubwa la makafiri hapa duniani lilikuwa ni kukusanya mali, kuwa na kazi, na watoto. Waliishi maisha yao wakitafuta malengo haya. Lakini siku ya kiyama watafahamu kwamba fikra hizi zote hazina thamani yoyote. Siku ya kiyama ni siku makafiri watatamani kutokomea. Lakini kwa upande wa waumini, ni wakati waliousubiri kwa hamu na gamu.Mwenyezi Mungu anaelezea haya katika aya hizi:

**Siku hiyo nyuso nyingine zitanawiri. Zitacheka, zitachangamka, na nyuso nyingine Siku hiyo zitakuwa na mavumbi juu yake, Giza Totoro litazifunika. Hao ndio makafiri watenda mabaya. (Surah Abasa: 38-42)**

Kwenye Siku ya Hesabu, vitu vya thamani mtu atakuwa navyo ni matendo mema yaliyofanywa kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini makafiri hawakufanya juhudi yoyote ya kupata thamani hii ambayo ingewapa uokovu wa milele. Hawana tendo hata moja zuri wataweza kuonyesha Siku hiyo kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hawakuwa na imani yoyote kwa Mwenyezi Mungu, matendo yote waliyoyatenda hayatakuwa na maana.

**Sema: Je! Tukujulisheni wenye hasara zaidi kwa vitendo (vyao)? Hao ambao bidii yao (hapa duniani) imepotea bure katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanafanya amali njema. Hao ni wale waliozikataa Ishara**

**za Mola wao na kukutana naye. Kwa hivyo vitendo vyao vimeharibika wala hatutawasimamishia mizani siku ya kiyama. (Surat al-Kahf: 103-105)**

Wale waliokanusha dini na kuwa na shaka kuwepo siku ya kiyama, hawakufanya matayarisho kwa siku hiyo. Kwa maisha yao yote walijishughulisha kutafuta mali na kufuata matamanio yao. Sasa wanakabiliana na majuto ambayo hawatawahi kujiondoa. Mwenyezi Mungu anataja katika Qurani Akisema:

**Wasema: "Ole wetu! Hii ndiyo (ile) siku ya Malipo! (Waambiwe) "Hii ndiyo siku ya Hukumu mliyokuwa mkiikadhibisha." (Surat as-Saffat: 20-21)**

La ziada ni kwamba makafiri watapata matendo yao yote ya ulaghai, ya kukosa shukrani na yote mabaya yatadhihirishwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Wao wenyewe watashuhudia madhambi waliyotenda. Mwenyezi Mungu Anaelezea katika Qurani kwamba:

**Na watahudhurishwa mbele ya Mola wako safu safu, (na wataambiwa): "Bila shaka mumetujia kama tulivyokuumbeni mara ya kwanza. Bali mlidhani ya kuwa hatukukuwekeni miadi (hii). Na daftari yatawekwa (mbele yao) ndipo utawaona waovu wanaogopa kwa sababu ya yale yaliyomo (daftarini); na watasema: "Ole wetu! Namna gani daftari hili! Haliachi dogo wala kubwa ili inalihesabu" na watakuta yote yale waliyoyafanya yamehudhurishwa hapo; na Mola wako hamdhulumu yoyote. (Surat al-Kahf: 48-49)**

**Siku hiyo watu watatoka (makaburini) vikundi – vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao. Basi anayefanya wema (hata ) sawa na chembe atauona. Na anayefanya uovu (hata) sawa na chembe atauona. (Surat az-Zilzal: 6-8)**

Kama vile anasimulia Mwenyezi Mungu katika Qurani, ni wakati wa makafiri kuona rekodi ya vitendo vyao.

Waumini watapata rekodi zao kwa upande wa kulia ilihali makafiri watapewa kwa upande kwa kushoto. Tangu wakati wa kutolewa roho, makafiri walipata adhabu kubwa na wakati wanapewa rekodi zao ni adhabu nyingine. Wanahepa kuangalia matendo maovu waliyotenda na wanatamani kupotea. Mwenyezi Mungu anaeleza katika aya hizi:

**Walakini atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kushoto basi yeye atasema: "Oo! Laiti nisingalipewa daftari langu. Wala nisingalijua ni nini hisabu yangu. Laiti (mauti ) yangemaliza (kila kitu changu). Mali yangu haikunifaa usultani (ukubwa ) wangu umenipotea." (Surat al-Haqqa: 25-29)**

**... Siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake miwili, na kafiri atasema: "Laiti ningalikuwa udongo!" (Surat an-Naba: 40)**

**Lakini atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake, basi yeye atayaita mauti na ataingia Motoni. Maana alikuwa na furaha pamoja na watu wake, (na) alidhani kuwa hatarejea (Kwa Mwenyezi Mungu) Kwa nini (asirejee) Mola wake alikuwa akimuona; (Surat al-Inshiqaq: 10-15)**

Makafiri wanaposhuhudia haya, wanafahamu fursa waliyopoteza wakiwa duniani na watahisi majuto makubwa. Kuongezea kwa majuto haya, ni pale wanapoona waumini wakistarehe peponi. Na hii ni kwa sababu waliitwa na waumini kwenye njia ya haki lakini walifunga masikio yao kwa ujeuri.

Lakini sasa "Mizani za uadilifu" (Surat al-Anbiya': 47) zimewekwa. Watu wataelekezwa Motoni au Peponi kulingana na vitendo vyao. Katika Siku ya Kiyama, makafiri wataona kule wanaelekea na hofu itawaingia:

**Utawaona (siku ya Kiyama) madhalimu wanavyotetemeka kwa sababu ya yale waliyochuma, nayo yatawatokea tu (Surat ash-Shura: 22)**

Uadilifu wa Mwenyezi Mungu utaenea na utakuwa wa kulipwa na pia kuadhibiwa.

**Nasi tutaweka mizani za uadilfu siku ya Kiyama, na nafsi yoyote haitadhulumiwa hata kidogo. Na hata kama ikiwa uzito mdogo wa chembe ya khardali nalo tutaileta; Nasi tunatosha kuwa wenye kuhisabu (Surat al-Anbiya': 47)**

Njia itakuwa nyepesi kwa waumini lakini ngumu sana na ya uchungu kwa makafiri. Wataulizwa kwa kila neema waliyopewa na Mwenyezi Mungu duniani. Watatoa hesabu ya wakati wao wote; ya kutofuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu; ya kutokuwa na shukrani; ya fikra mbovu na matusi; onyo walizopuuza. Zile udhuru walizozitoa duniani hazitakubaliwa kamwe. Mwenyezi Mungu Anaeleza hali makafiri watakuwemu siku hiyo Akisema:

**Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha! Hii ni siku ambayo hawatasema (kitu) Wala hawatapewa ruhusa (kutoa udhuru) wakapata kutoa. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha! (waambiwe) : "Hii ni siku ya Hukumu, tumekukusanyeni nyinyi na waliotangulia. Ikiwa mnayo hila ifanyeni juu yangu." Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha! (Surat al-Mursalat: 34-40)**

Wale makafiri ambao hawatakuwa na matendo mema mbele ya Mwenyezi Mungu "watajua walichotayarishiwa. Mwenyezi Mungu Anaeleza pahali hapa adhabu kama shimo lisilo na mwisho.

**Basi Yule ambaye mizani yake itakuwa nzito, huyo atakuwa katika maisha yanayompendeza. Na yule ambaye mizani yake itakuwa nyepesi, huyo maskani yake yatakuwa katika (huo Moto)-Hawiya. Na ni jambo gani litakalokujulisha ni ni hiyo (Hawiya)? Ni Moto uwakao kwa ukali. (Surat al-Qari'a: 6-11)**

Ni muhimu kufahamu majuto makubwa watakayohisi makafiri siku ya Kiyama. Yeyote atakayejuta siku ya Kiyama atakuwa ni wa kuchelewa sana. Yeyote atakayefahamu haya na bila kupoteza wakati akaanza kutenda mambo mema, ataweza kutarajia "Mizani nzito (ya matendo mema) ni hiyo tu itakayoweza kumuokoa mtu kwa majuto makubwa.

# Majuto kwenye Jahannam

## (Moto huo) utakapowaona tangu katika mahali pa mbali, watasikia hasira (yake) na mngurumo (wake) (Surat al-Furqan: 12)

**Majuto watakuyokuwa nayo makafiri watakapouona Moto**

Hesabu ikishakamilika siku ya Kiyama, watu watakusanywa na kupelekwa Motoni kwenye vikundi. Miongoni mwao watakuwa ni wale walikadhibisha dini na kukataa kuwepo Mwenyezi Mungu na wale walikataa ishara za Mwenyezi Mungu kwa ujeuri. Kutakuwa na wale walifurahia mali na ufahari. Kwa masikitiko vile vitu walivipa umuhimu duniani havitawafaa na kuwaondolea adhabu ya milele. Mwenyezi Mungu anatufahamisha kwenye Qurani kwamba makafiri wote wataingizwa Motoni kwa fedheha. Wenye kuchunga Moto, watawafanya makafiri wakiri makosa yao kwa mara ya mwisho na kuwaingiza ndani. Mwenyezi Mungu kwenye Qurani anaeleza namna makafiri watapelekwa Motoni:

**Na waliokufuru watapelekwa katika Jahanamu makundi kwa makundi; mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake; na walinzi wake watawaambia: "Je! Hawakukujieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni Aya za Mola wenu na kukuonyeni mkutano wa siku yenu hii?" watasema: ndiyo, Lakini limetimia neno la adhabu juu ya makafiri. Itasemwa: "Ingieni milango ya**

**Jahanamu mkakae humo." Basi ni ubaya ulioje wa makazi ya wanaotakabari! (Surat az-Zumar: 71-72)**

**"Haya ni kwa sababu mlikuwa mkifurahi katika ardhi pasipo haki, na kwa sababu mlikuwa mkijivuna. Ingieni katika milango ya Jahanamu mkakae humo milele; basi ni mabaya yalioje makazi ya wanaotakabari!" (Surah Ghafir: 75-76)**

Hakuna mtu yeyote kwenye kikundi atasimama kusema hakuonywa kutokana na hii siku. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ambaye ni muadilifu, aliwatuma mitume kwa kila mtu kumkumbusha kuhusu kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, siku ya Kiyama, Pepo na Jahanam. Kwa hivyo, makafiri watakiri kwamba wanastahiki adhabu ya Jahanam.

Walikuwa na kiburi mbali na kuwa walionywa na pia walikataa kumuabudu Mwenyezi Mungu, Yule aliyewaumba, Mwenyezi Mungu Anamjulisha mwanadamu kenye Quran kwamba watu aina hii watadhalilishwa kwenye Jahanam.

**Na Mola wenu anasema: "niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajuvunao kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia Jahanamu, wakifedheheka. (Surah Ghafir: 60)**

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saas) pia amesisitiza nukta hii akisema :

*Je! Niwajulisheni watu wa Motoni? Itakuwa na kila katili, kila mwenye vurugu, mwenye kiburi na kila mwenye kujivuna (Bukhari)*

Walijiona kama wenye nguvu duniani na wakamuasi Mola wetu. Walidhani usultani utawaokoa. Walipokumbushwa kuhusu sifa ya Mwenyezi Mungu ya al-Qahhaar ( Mwenye Nguvu), kuwepo Moto na Pepo, na kuelezwa kufuata njia ya Mwenyezi Mungu walijibu:

**"Mbona Mwenyezi Mungu hatuadhibu kwa haya tunayoyasema?" Basi (moto wa) Jahanamu utawatosha kuwatia adhabu; watauingia; napo ni mahali pabaya sana pa kurudia. (Surat al-Mujadala: 8)**

Kwa sababu ya kuasi kwao, wataingizwa kwenye milango ya Moto na hawataweza kutoka humo isipokuwa Mwenyezi Mungu Akipenda kuwaondoa. Wakati wanapoona moto, watahisi majuto makubwa kwa makosa yao. Mwenyezi Mungu Anaeleza kwenye Qurani kwamba huu ndio wakati watafahamu kwa uwazi kwamba hakuna njia ya kutoka nje ya Moto.

**Na wabaya watauona Moto (wakti huo) na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka. (Surat al-Kahf: 53)**

Makafiri wataona ukweli ukiwa wazi wakiwa Motoni, chochote walichojisahaulisha duniani kitakuwa wazi kwao. Watafahamu kuwa waliishi maisha yao kwa malengo ya upuzi na hatimaye watatambua kwamba maisha mafupi ya raha

waliyopata duniani ni lazima sasa kuishi kwenye adhabu isiyo na mwisho. Muda walioishi duniani ulionekana mrefu kwao lakini hawakutafakari kuhusu maisha ya akhera. Hawakujiandaa kwa maisha ya akhera ambayo hayana udhaifu wa mwili, njaa au uchovu lakini wao walichagua maisha ya duniani ambayo hayana raha. Wanapoingia kwenye milango za Moto wanafahamu kwamba hakuna kuepuka. Na wanadhani kwamba wanaweza kutoa fidia ya kila walichokuwa nacho duniani ili kuokoa nafsi zao. Lakini juhudi zao za upuzi zinaelezwa ifuatavyo:

**… Na wale wasiomuitikia, hata kama wangalikuwa na vyote vilivyomo ardhini na (vingine) kama hivyo pamoja navyo, bila shaka wangalivitoa kujikombolea. Hao watakuwa na hisabu mbaya, na makao yao ni Jahanamu. Na ni mahali pabaya palioje! (Surat ar-Rad: 18)**

Lakini, juhudi hizi za mwisho zitaambulia patupu wakati wa kuingia Motoni. Mwenyezi Mungu Anatufahamisha kwamba majaribio hayo hayatakuwa na faida yoyote.

**“Basi leo hakitapokelewa kwenu kikomboleo wala kwa wale waliokufuru. Makazi yenu ni Motoni; ndio rafiki yenu; nayo ni marejeo mabaya kabisa.” (Surat al-Hadid: 15)**

Kwa hakika kuna sababu inayofanya majaribio hayo yasiwe na manufaa. Mwenyezi Mungu Aliwaonya kuwa kuna Moto walipokuwa duniani. Kila kitu kiliwekwa wazi kwamba hakuna mtu atasaidia mwengine na hakuna atakayeweza kutoa fidia. Aya ambayo Mwenyezi Mungu aliteremsha kuelezeza hoja hii ni:

**Na iogopeni Siku ambayo nafsi haitafaa nafsi nyingine cho chote, wala hayatakubaliwa kwake maombezi, wala hakitapokewa kikomboleo kwake; wala hatanusuriwa. (Surat al-Baqara: 48)**

Licha ya onyo zote, walisisitiza kukadhibisha kwao na kwa hivyo walijiandalia mwisho huu mbaya. Siku hiyo watakiri kwamba matendo yao yaliyowafanya kuingia Motoni.

Majuto hayo yatakuwa ni ya adhabu ya milele bila kuokolewa isipokuwa kutaka kwa Mwenyezi Mungu. Na watajua nukta muhimu; kwamba lau wangejitolea maisha yao kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu badala ya kufuata malengo duni, wangeingizwa Peponi badala ya Motoni. Kwa sababu ya kutofuata njia sahihi wanapata hasara kubwa.

Mwenyezi Mungu Anataja kwenye aya ya ishirini ya Surat al-Balad “Moto uliofungiwa (kila upande) utakuwa juu yao.” wanapoingia kwenye milango za Moto, watafungiwa ndani. Na mbele ya milango hizo ni adhabu ya Motoni isiyokuwa na mwisho na wataadhibiwa hadi pale anapotaka Mwenyezi Mungu. Kwa makafiri hakuna njia ya kuihepa adhabu hiyo. Mwenyezi Mungu Anauita moto huo ‘Huthwama’

**Na ni jambo gani litakalokujulisha ni nini Huthwama? Ni Moto wa Mwenyezi Mungu uliowashwa.ambao unapanda nyoyoni. Hakika huo (moto) watafungiwa. Kwa magogo marefu marefu . (Surat al-Humaza: 5-9)**

**Adhabu wanayokumbana nayo makafiri Motoni**

Kabla hatujataja majuto watakayokumbana nayo makafiri akhera, itakuwa vyema kueleza adhabu ya Motoni. Bila kufahamu aina ya adhabu Motoni, mtu anaweza kughafilika kiwango cha majuto yaliyomo.

Kama tulivyotaja hapo awali, majuto ya makafiri yanaanza pindi wanapouona Moto na majuto ya milele. Mazungumzo baina yao wakiingia Motoni yatakuwa hivi:

**Na waliomkufuru Mola wao iko adhabu ya Jahanam (inawangojea) na ni marejeo mabaya yalioje! Watakapotupwa humo watasikia rindimo (mngurumo) lake, nalo lafoka. Unakaribia kupasuka kwa hasira . kila mara litakapotupwa humo kundi (la wabaya ) walinzi wake watawauliza: "Je! Hakuwafikieni Muonyaji? Watasema : "Kwa nini? Alitujia Muonyaji, lakini tulimkadhibisha na tulisema "Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote, nyinyi hamumo ila katika upotofu mkubwa. Na watasema : " kama tungalikuwa tunasikia au tungalikuwa na akili hatungekuwa katika watu wa Motoni. Wakakiri dhambi zao; basi kuangamia kumewastahikia watu wa Motoni (Surat al-Mulk: 6-11)**

Kama vile imetajwa kwenye aya, watakaporushwa kwenye Moto, watasikia mngurumo. Mwenyezi Mungu Anaeleza mngurumo huo kwenye aya ya saba ya Surat al-Mulk kama **mngurumo unaofoka**

Mngurumo huo utawaingiza hofu kwa makafiri. Katika aya nyingine Mwenyezi Mungu anaeleza kuwa Moto wa jahanam kuwa moto unaokaribia kupasuka kwa hasira (Surat al-Mulk: 8).

Watakuwa kwenye hali ya taharuki kwani watafahamu kwamba adhabu watakayoipata itakuwa ya kutisha na ya uchungu, imeelezwa kwamba Jahanam ni pahali pabaya pa kuishi.

**.....napo ni mahala pabaya pa kurejea (Surah Al 'Imran: 162)**

**Napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia (Surat an-Nisa: 115)**
**Na makazi yao yatakuwa Motoni, na ni mabaya yalioje maskani ya madhalimu. (Surah Al 'Imran: 151)**
**Jahannamu, wataingia; na ni mahali pabaya kabisa pa kukaa (Surah Ibrahim: 29)**

Mtume (S.a.a.s) pia ameelezea Jahannam kwenye hadithi zake tukufu kwamba:

*Miongoni mwa watu wa Jahannam ni wale wataingizwa motoni hadi kwenye vifundoni vyao , wengine hadi kwenye magoti, wengine hadi viuno na wengine hadi kwenye koo zao . (Muslim)*

Wakazi wa Motoni watatupwa mahala hapa pabaya kwa umati. Katika aya inasema "**Basi watatupwa humo wao na waaasi** (wengine) (Surat ash-Shu'ara: 94)

Hawatapata heshima yoyote Motoni wala rahma. Watakuwa kuni za Moto na wataishi kwenye maumivu na huzuni milele. Mwenyezi mungu anazungumzia haya kwenye aya hizi:

**Hakika nyinyi na wale mnaoabudu, kinyume cha Mwenyezi Mungu, ni kuni za Jahannamu; mtaifikia. (Surat al-Anbiya': 98)**

**… Na hao (watakuwa) kuni za Moto (Surah Al 'Imran: 10)**

Mwenyezi Mungu anatufahamisha kwenye Qurani sampuli za adhabu Motoni. Wengi wa watu wataishi humo milele kumaanisha wataadhibiwa namna atataka Mwenyezi Mungu. Tunaweza kueleza aina za adhabu kama :

Katika aya ya kumi na tatu ya Surat al-Furqan, Mwenyezi Mungu Anaeleza kwamba makafiri watatupwa "mahala pafinyu hali wamefungwa" kwa hakika kufungwa mahala finyu hata kwa dakika chache kunamfanya mtu kuhangaika. Kidogo unaweza kufananisha na kufungiwa kwa chumba kunahofisha katika dunia. Lakini huwezi kufananisha adhabu ya duniani na ile ya akhera. Watakapofungiwa katika mahala finyu, watapata adhabu ya moto. Na vile watakuwa wamefungwa pamoja hawataweza kusongea na kuhepa kutoka kwenye moto haitowezekana. Kujaribu kutafakari kuhusu kisa hiki kunaleta uchungu

Katika aya nyengine Mwenyezi Mungu anawajulisha makafiri kwamba watabaki kwenye "**kivuli cha moshi mweusi sana**" (Surat al-Waqia: 43). Kwa kawaida neno kivuli kinakuwa ni cha kutuliza. Lakini ni kinyume sana kwenye Moto ambako Mwenyezi Mungu Anatujulisha kwamba kivuli hicho si baridi wala cha starehe.

Aina nyingine ya adhabu katika Jahannam ni kukosekana mauti. Kifo ni njia moja ya kuokolewa. Kwa sababu hii Mwenyezi Mungu hatakubali watu wa Jahannam kufariki kama vile anasisitiza katika aya "**na mauti yatamjia kutoka kila mahali, naye hatakufa**" (Surah Ibrahim: 17).

Mtume Muhammad (s.a.a.s) pia amesimulia kuwa hakuna mauti akhera akisema:

*Watu wa peponi watakapoelekea Peponi nao wa Motoni kuelekea Motoni, mauti yataitwa na kuwekwa baina ya Pepo na Moto. Kisha itatangazwa: "Enyi watu wa Peponi! Hakuna mauti tena! Enyi watu wa Motoni! Hakuna mauti tena! Hili litaongeza furaha kwa watu wa Peponi na kuongeza huzuni kwa watu wa Motoni (Muslim)*

Katika dunia kuchomwa na moto mkali kunamletea mtu mauti baada ya muda mfupi. Hakuna anayeweza kustahmili moto. Na kama mtu huyo hatakufa na kupata majeruhi peke yake, itachukuwa muda mrefu vidonda kupona vizuri. Lakini katika Motoni, adhabu ya Motoni haina mfano wa moto tunaoujua duniani. Katika Motoni, ngozi zitabadilishwa tena ili kuonja adhabu kali tena. (Surat an-Nisa: 56). Kwa ufupi, watu wa Motoni watapata adhabu ya milele inayosababishwa na Moto hadi kupenda kwa Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu anaelezea aina nyingine ya adhabu inayosababishwa na moto katika aya ya kumi na tatu ya Surat adh-Dhariyat anaposema watu wa Motoni wataadhibiwa na moto. Ni vigumu kuelewa uchungu huo. Ukizingatia kuwa uchungu mdogo anaoupata mwanadamu hapa duniani, anaweza kufahamu mauvimu hayo.

Mwanadamu pia atapata yafuatayo:

**Tena katika mnyororo wenye urefu wa dhiraa sabini muingizeni (Surat al-Haqqa: 32)**

**Hakika sisi tumewaandalia makafiri minyororo na makongwa na Moto mkali (Surat al-Insan: 4)**

**Na kwa ajili yao (yatakuwapo) marungu ya chuma (Surat al-Hajj: 21)**

**Siku yatakapotiwa moto katika moto wa Jahanamu, na kwa hayo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu na migongo yao.**

**Yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yachemkayo. (Surat al-Hajj: 19)**

**Nguo zao zitakuwa za lami, na Moto utazijaa nyuso zao. (Surah Ibrahim: 50)**

Hawatapata kinywaji cha kustarehesha. Siku hiyo ni maji moto (Surat al-Sad: 57) damu na usaha (Surat al-Haqqa: 36) ndio vinywaji vyao.

Na chakula cha watu wa Motoni ni matunda machungu ya mti wa zakkum. Mwenyezi Mungu vipi zaqqum itakuwa adhabu kwa makafiri:

**Bila shaka mti wa Zakkum ni chakula cha waasi, (kwa joto lake ni) kama shaba iliyoyayushwa, huchemka matumboni, kama mchemko wa maji ya moto. (kuambiwe) "Mkamateni (huyo asi) na mbururemi mpaka katikati ya Jahanamu. Kisha mwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji ya moto. Onja! Ulikuwa (ukijidai kuwa) wewe ni mwenye nguvu, mhishimiwa! Hakika hii ndiyo ile (adhabu) mliyokuwa mkibishana" (Surat ad-Dukhan: 43-50)**

Kutokana na maelezo ya Qurani, tunafahamu kwamba chakula cha Motoni kitakuwa cha kusonga. Watajaribu kunywa maji kwa pupa lakini hawataweza kumeza. Usaha ambao ni kitu kisichopendeza kabisa hapa duniani kwa rangi, ndio chakula cha watu wa Motoni. Hii itakuwa na machungu makubwa lakini kwa kukosa hiari hawatakuna na budi ila kula hivyo hivyo ingawa watakachokula hakitawafaa kwa njaa yao na watakuwa na uchungu wa njaa kwa milele.

**Hawatakuwa na chakula isipokuwacha miba. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa. (Surat al-Ghashiyya: 6-7)**

Mwenyezi Mungu anaelezea pahala pengine kwenye Qurani kuhusu adhabu ya Motoni akisema:

**Wao humo watapiga kelele, (Surat al-Anbiya': 100)**

**Wakae humo dahari nyingi (karne baada ya karne). (Surat an-Naba: 23)**

**Humo watakaa milele. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi ya (ya kupumzika) ... (Surah Al 'Imran: 88)**

**Watataka watoke katika Moto, lakini hawatatoka humo. (Surat al-Maida: 37)**

Kwa hakika adhabu hiyo itakuwa ni ya uchungu mkali na majuto kwa makafiri. Ili kutaka kuokolewa wataomba mara nyingi na watakuwa radhi roho zao kutolewa. Mwenyezi Mungu katika Qurani tukufu Anatufahamisha mazungumzo ya watu wa Motoni akisema:

**Na watapiga kelele (kumwambia Yule Malaika anayewaadhibu waseme): Ee Malik! Naatufihse Mola wako!" (Malik )_aseme: "Bila shaka mtakaa humu humu. Kwa yakini tulikuleteeni haki, lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia haki." (Surat az-Zukhruf: 77-78)**

Kuipa dini mgongo na kukosa kusikiza onyo itakuwa ndio sababu ya kuangamia kwa watu hawa kama vile amesimulia Mwenyezi Mungu katika Qurani. Mwenyezi Mungu naye hatasikiza vilio vyao na atawaweka kwenye adhabu hadi atakapotaka.

Hizi ni baadhi ya adhabu watakazopata wale walimkadhibisha Mwenyezi Mungu na kuwepo Jahanam na Pepo. Na makafiri watakuwa na aina nyingine ya adhabu ambayo ni hisia ya majuto ambayo hakuna atakaye weza kusahau. Na hisia hizi zitaongezeka pale watakapoona kwamba wanapelekwa Motoni, pahala pa kutisha sana. Kama vile imesemwa awali, kila makafiri wataonja adhabu, watakumbuka kwamba lau wangefuata njia ya haki, haya yote hayangewapata lakini hakuna njia ya kuepuka majuto haya.

**Majuto ya Makafiri kwenye Moto**

Wakati makafiri wanapata adhabu kali, watakuwa na majuto ya kutoamini kwa Mwenyezi Mungu walipokuwa duniani. Kwa bahati mbaya majuto haya hayatakuwa na faida yoyote. Walipokuwa duniani walipewa fursa nyingi ambazo hawakutumia. Wakati watafahamu haya, watalaumu kila mtu na kila kitu kilichowazuia kuamini kwa Mwenyezi Mungu na siku ya Kiyama na kuwafanya wapende mambo ya dunia sana

Kulingana na Qurani makafiri watakuwa na hasira kubwa kama vile Mwenyezi Mungu anasema kwenye aya zifuatazo:

**Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwapinduliwa (zitakapounguzwa ) Motoni, waseme: "Laiti tungemtii Mwenyezi Mungu na tungemtii Mtume." Na watasema: "Mola wetu! Hakika tumewafuata mabwana wetu na wakubwa wetu, basi wao wametupoteza njia. Mola wetu! Wape hawa adhabu maradufu na uwalaani laana kubwa." (Surat al-Ahzab: 66-68)**

**Hata atakapotujia atasema (kumwambia shetani): "Laiti ungalikuwa umbali wa mashariki na magharibi baina yangu na wewe." Na rafiki mbaya ulioje wewe! (Na Mwenyezi Mungu atawaambia): "Haitakufaeni leo- mlivyodhulumu (nafsi zenu)- kwamba nyinyi mnashirikiana katika adhabu. (Surat az-Zukhruf: 38-39)**

Kama vile aya hizi zinaashiria, makafiri wanafikiri wataokolewa kwa kulaumu wale waliowapotosha kutoka kwa njia ya haki. Lakini ukweli ni kwamba Mwenyezi Mungu alimpa kila mtu ubainifu wa kujua njia ya haki. Na pia Mwenyezi Mungu amempa binadamu hiari ya kuamua. Kwa hivyo, mwanadamu amepewa chaguo mbili na elimu ya kujua la kweli na lisilo la ukweli na hivyo basi ni juu yake kuchagua analolitaka. La muhimu ni kwamba Mwenyezi Mungu anajua imani ya mtu au ukafiri wake kwenye moyo wake. Kwa hivyo wale wanaofanya wengine kuingia Motoni na wale wanowafuata wataadhibiwa kwa uadilifu. Siku hiyo hakuna atakaye beba mzigo wa mtu mwingine.

Wakati ule watu hawa walikuwa wakishawishi na kutenda maovu na haikuwajia kwamba siku moja watahukumiwa siku ya Kiyama na hawakuzingatia kabisa. Walihimizana kumkadhibisha Mwenyezi Mungu wakisema, "Nitachukua jukumu la kila unalolifanya" naye Shetani kwa upande mwingine aliwashawishi na kuwaahidi na kuwapotosha. Lakini Mwenyezi Mungu kakita ayah hii , **"... na atatujia peke yake**." (Surah Maryam: 80), anatufahamisha kwamba ahadi hizo hazitakuwa na maana.

Siku hiyo makafiri watajiona wakiwa peke yao. Watafahamu jambo la muhimu: mbali na Mwenyezi Mungu binadamu hana rafiki wala mlinzi. Wakiwa Motoni wale watu waliowachukulia ndio wakufunzi wao au marafiki wakiwa duniani

watawaacha peke yao. Vile vile shetani, ambaye alimuasi Mwenyezi Mungu , atawakataa na kuwaambia:

**Na shetani atasema itakapokatwa hukumu "Mwenyezi Mungu alikuahidini ahadi ya kweli (na leo ameitimiza), nami nilikuahidini; lakini sikukutimizieni. Wala sikuwa na mamlaka juu yenu (ya kukulazimishieni kunifuata), isipokuwa nilikuiteni tu, nanyi mkaniitika. Siwezi kukusaidieni wala nyinyi hamuezi kunisaidia. Hakika mimi nilikataa kunishirikisha kwenu kutoka zamani." Kwa yakini madhalimu watakuwa na adhabu iumizayo. (Surah Ibrahim: 22)**

Hivyo ndivyo itaonekana ukosefu wa uaminifu kwa wale waliowachukua kama marafiki ni hii itakuwa yaongeza majuto kwa makafiri. Je! Hawaoni kwamba hakuna wa kumkimbilia isipokuwa Mwenyezi Mungu. Lakini watakapojua kuwa kufahamu hili halitawapunguzia shida zao watakereka zaidi. Siku hiyo watagombana wao kwa wao wakikiri madhambi yao. Mwenyezi Mungu anaeleza haya kwenye aya hii:

**Watasema: (kuwaambia wale waliokuwa wakiwaabudu) – na hali ya kuwa wagombana humo. "Wallahi, kwa yakini tulikuwa katika upotofu ulio dhahiri. Tulipokuwa tukikufanyeni sawa na (Mwenyezi Mungu) Mola wa walimwengu wote. Na hawakutupoteza ila wale waovu; basi hatuna waombezi, wala rafiki halisi. Laiti kama tungalikuwa na marejeo (ya kurejezwa ulimwenguni) tungekuwa miongoni mwa waumini." (Surat ash-Shu'ara: 96-102)**

Kama vile imeelezwa hapo juu kwenye aya, makafiri, kwa majuto makubwa, watatamani kurejeshwa duniani ili wafanye matendo mema ambayo yatawaletea manufaa akhera. Lakini, ni matamanio yasiyokubalika. Watafahamu kwamba kila kitu walichokimbilia duniani hakina maana ikiwa ni utajiri, urembo, kazi n.k Mwenyezi Mungu anaeleza kwenye Qurani majuto ya makafiri Akisema:

**Walakini atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kushoto basi yeye atasema: "Oo! Laiti nisingalipewa daftari langu; wala nisingalijua ni nini hisabu yangu, laiti (mauti) yangemaliza (kila kitu changu), mali yangu haikunifaa, usultani (ukubwa) wangu umenipotea (kusemwe) : "Mkamateni na mtieni makongwa, kasha mtupeni Motoni, tena katika mnyororo wenye urefu wa dhiraa sabini muingizeni. Hakika yeye alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wala hahimizi kulisha maskini. Basi leo hapa hana rafiki mpenzi. (Surat al-Haqqa: 25-35)**

**... Basi Siku hiyo italetwa Jahanamu. Siku hiyo mwanadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini? Atasema: "Laiti ningalitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo)"**

Vile vile makafiri watakapoona watu wa Peponi wana furaha kubwa, majonzi na masikitiko yao yataongezeka. Wataona tofauti kubwa ya maisha ya watu wa Peponi na yao. Mwenyezi Mungu Anatuonyesha tofauti ya watu wa Peponi na watu wa Motoni.

Mwenyezi Mungu Anatuelezea kwenye Qurani hali ya watu wa Motoni akisema:

**Macho yao yatainama chini, unyonge utawafunika. (Surat al-Qalam: 43)**

**Na nyuso siku hiyo zitakunjana. (Surat al-Qiyama: 24)**

Kwa upande Mwingine Mwenyezi Mungu Anawasifu watu wa Peponi Akisema:

**Siku hiyo nyuso nyingine zitanawiri, zitacheka, zitachangamka (Surah Abasa: 38-39)**

Chakula cha makafiri kitakuwa ni maji moto, usaha, miiba chungu, na mti wa zaqqum. Lakini kwa upande mwingine, waumini watatuzwa mito ya maziwa na asali, vinywaji vitamu kwenye vikombe, aina yote ya matunda na chochote watakacho. Katika aya hii, Mwenyezi Mungu Anasifu chakula cha watu wa Peponi Akisema:

**Mfano wa Pepo waliyoahidiwa watawa (wacha Mungu itakuwa hivi): imo mito ya maji yasiyovunda, na mito ya maziwa isiyoharibika ladha yake, na mito ya ulevi wenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyosafishwa; tena humo watapata matunda ya kila namna, na msamaha kutoka kwa Mola wao. Basi hao watakuwa sawa na wale watakaokaa Motoni? Na kunyweshwa maji yachemkayo yatakayokata matumbo yao. (Surah Muhammad: 15)**

Kwa hakika huwezi kulinganisha neema wanazopewa waumini na chakula cha makafiri ambacho hakiondoi njaa bali ndio chanzo cha adhabu ya milele. Watakuwa kwenye moto kwa karne; ngozi zao zitabadilishwa baada ya kuchomwa; wataomba kupunguziwa na kupewa starehe. Watamani neema wanazopata watu wa Peponi ambao wamestarehe kwenye kivuli na watajiombea. Mola wetu Anasimulia haya kwa Qurani tukufu Akisema:

**Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi, (kuwaambia): "tumimieni maji au katika vile Alivyokupeni Mwenyezi Mungu." Waseme (watu wa Peponi): "Hakika Mwenyezi Mungu Ameviharamisha vyote viwili hivyo kwa makafiri." (Surat al-Araf: 50)**

Mwito wa makafiri hautaitikiwa. Mwenyezi Mungu Anasisitiza hili kwenye aya hii:

**....Hakika tumewaandalia madhalimu moto ambao kuta zake zitawazunguka. Na wakiomba msaada (kwa kiu kikubwa kilichowashika) watasaidiwa kwa (kupewa) maji kama ya shaba iliyoyayushwa itayoziunguza nyuso (zao). Kinywaji kibaya kilioje hicho! Na mahala pabaya palioje! (Surat al-Kahf: 29)**

Vile vile, Mwenyezi Mungu Atawatuza watu wa Peponi nguo za kijani za hariri nyororo, jamdani la fakhari, bangili za dhahabu na fedha. Lakini kwa upande mwingine, makafiri watakuwa na nguo za lami na moto walizotengezewa. Waumini wataishi kwenye makao mazuri na vyumba vya kifahari, wakiegemea jamdani la fakhari lakini makafiri makao yao yatakuwa ni Jahanam itakayofunikwa na safu.

Mwenyezi Mungu Anatufahamisha kwenye Qurani kwamba waumini watapata kila watakacho na watu wa Peponi watakirimiwa kwa maisha ya raha na amani Peponi.

**Watapata watakayotaka kwa Mola wao. (Surat ash-Shura: 22)**

**Basi Mwenyezi Mungu Atawalinda na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha. (Surat al-Insan: 11)**

Kama makafiri wangewajibika na kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa moyo msafi, hawangepata adhabu ya Jahannam siku hiyo. Kwa hivyo masikitiko ya makafiri yanaongezeka wanapoona watu wa Peponi. Mwenyezi Mungu anaeleza adhabu wanayoipata na majuto wanayosikia kama "mateso" na kila mara makafiri watajaribu kukimbia mateso wataongezewa adhabu nyingine:

**Kila mara watakapotaka kutoka humo (adhabuni) kwa sababu ya uchungu, (maumivu) watarudishwa mumo humo na (kuambiwa): "Ionjeni adhabu ya kuungua."**

Hii ni kwa sababu hakuna kujitoa kwenye Jahannam. Ni mahala ambapo hisia za kujuta hazimfaidi yeyote. Vile vile kwenye Jahannam fikra ya majuto haijabainishwa. Wakati makafiri wanaaga dunia, malaika watawaambia hawatawahi kuonja uzuri hadi milele isipokuwa kutaka kwa Mwenyezi Mungu.

**Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wenye makosa na watasema: (Mungu) atuepushie mbali adhabu hii iliyotukabili." (Surat al-Furqan: 22)**

Makafiri wataona njia peke ya kusalimika kwao ni kuangamizwa kabisa. Wataomba kuangamizwa lakini haitawezekana. Hii ni kwa sababu walipewa umri mrefu wa kupata mawaidha lakini wao walikataa na kukengeuka ukweli. Mwenyezi Mungu atawajibu akisema:

**"Msiyaite leo mauti mamoja bali yaiteni mengi." (Surat al-Furqan: 14)**

**"Uingieni, mkistahamili au msistahamili, ni mamoja kwenu; mnalipwa mliyokuwa mkiyatenda." (Surat at-Tur: 16)**

Katika aya ya arubaini ya Surat al-Araf, Mwenyezi Mungu anaeleza kutowezekana kwa makafiri kutolewa Motoni na kuingizwa Peponi akisema "hawataingia Peponi mpaka aingie ngamia katika tundu la sindano." Na kisha Mwenyezi Mungu anasema makafiri watasahaulika kwa sababu wakiwa duniani walienda kinyume na hakina kupuuza kukutana Siku ya Kiyama. Hawatapata mwitikio wala msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

**Atasema "Ndivyo vivyo hivyo. Zilikujia Aya Zetu ukazisahau, (ukazipuza), na kadhalika leo utasahauliwa." (Surah Taha: 126)**

**Na itasemwa: "Leo tunakusahauni (Motoni) kama nyinyi mlivyosahau siku yenu hii; na mahali penu ni Motoni, wala hamna wa kukunusuruni." (Surat al-Jathiyya: 34)**

**Ambao walifanya dini yao kuwa upuzi na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganyia. Basi leo Sisi tunawasahu kama walivyosahau mkutano wa siku yao hii, na kwa sababu ya kule kuzikataa Aya zetu. (Surat al-Araf: 51)**

Watamsihi na kumuomba Mwenyezi Mungu awaondoe kwenye moto na Mwenyezi Mungu atawajibu hivi:

**" Mola Wetu! Tutoe humu (Motoni, uturejeshe ulimwenguni, tukafanye amali nzuri); na tufanyapo tena bila shaka tutakuwa madhalimu ( wa nafsi zetu kweli kweli)."**

Makafiri watapata adhabu kali na hawatapata msaada wowote kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hatawaonyesha huruma yake, wala ulinzi wowote na pia hatawasamehea madhambi na makosa yao. Kama wangemrudia Mwenyezi Mungu wakati wangali duniani wangelimpata Mwenyezi Mungu Mwingi wa msamaha na Mwingi wa huruma kwao. Lakini pindi wanapoingia Motoni kujua hilo halitawasidia kamwe.

Baada ya kusema haya yote, ni lazima kila mtu azingatie haya : kwamba Mwenyezi Mungu ni mwingi wa rehema kwa waja wake na binadamu anahitajia Mwenyezi Mungu peke yake awe rafiki na mlinzi wake. Mtu akishafungiwa milango za Jahanam nyuma yake, hazitafunguliwa hadi Mwenyezi Mungu atataka na hatapata fursa kama aliyoyipata akiwa duniani. Katika Qurani, Mwenyezi Mungu anaeleza kuwa kuokoka ni kama ifuatavyo:

**Isipokuwa wale waliotubu na wakajitengenezea na wakamshika Mwenyezi Mungu na wakaukhalisisha utii wao kwa Mwenyezi Mungu, basi hao wako pamoja na Waislamu waumini . Na Mwenyezi Mungu atawapa ujira mkuu waumini. Mwenyezi Mungu hakuadhibuni kama mtashukuru na mtaamini. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea shukrani ndiye Mwenye kujua. (Surat an-Nisa: 146-147)**

## Je! Vipi kuepuka majuto Siku ya Kiyama?

**Mwenyezi Mungu hakuadhibuni kama mtashukuru na mkaamini. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea shukrani ndiye Mwenye kujua. (Surat an-Nisa: 146-147)**

Binadamu wameumbwa kwa udhaifu na kutokamilika. Katika umri wetu, tunasahau mambo mengi na kufanya makosa mengi. Lakini kupitia kuomba msamaha ambao Mwenyezi Mungu ametupa kama fadhla kubwa tunaweza kurekebisha makosa yetu. Kwa hakika huo ndio msingi wa maisha ya duniani: tunafundishwa, tunatahiniwa, na kutakaswa makosa yetu. Yawezekana kwamba tunajuta makosa yetu au namna tumeendesha maisha yetu. Lakini tunaweza kurekebisha kwa kuomba msamaha na kutarajia kusamehewa na Mwenyezi Mungu.

Katika Qurani, Mwenyezi Mungu anatoa bishara kwamba Atasamehe madhambi ikiwa mtu ataomba msamaha kwa dhati. Mwenyezi Mungu anajua fikra zetu na kila neno tunaloficha. Anajua ikiwa tuko wakweli au la. Mwenyezi Mungu anaonyesha ukaribu wake na waja wake akisema:

**Mola wenu anajua sana yaliyo nyoyoni mwenu Kama mkiwa wema. Kwani Yeye ni Mwenye kuwaghufiria wenye kurejea (kwake) (Surat al-Isra: 25)**

Lakini linalojitokeza ni kwamba, baada ya kifo, haitawezekana kurekebisha makosa na madhambi yaliyofanywa duniani isipokuwa atakavyotaka Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo tusipoteze muda wetu hada kidogo. Madakika yanasonga kwa kufumba na kufumbua macho na kila muda unaposogea, tunakaribia mauti. La kuzingatia ni kwamba hatuwezi kujua wakati wa kifo utakapowadia. Siku, saa na dakika haijulikani. Hatimaye sote tutafariki na lazima tutoe hesabu ya vitendo vyetu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo binadamu lazima azingatie kuwa anaweza kufariki wakati wowote. Ikiwa hataki kujuta akiwa akhera, ni lazima atafakari kuhusu maisha yake.

Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wetu na kila linalotakikana kwa mtu mbele ya Mwenyezi Mungu ni kutekeleza

wajibu wake kama mja wakati akiwa duniani. Muumin hutekeleza wajibu wake wa dini ipasavyo, anasimamisha swala tano kwa furaha, kufanya wudhu, kufunga kama vile ameamrishwa na Mwenyezi Mungu kwa maisha yake yote.

Ameripoti Ibn 'Umar (ra):

*Mtume (s.a.a.s) amesema: "Dini ya Uislamu imejengwa kwa misingi tano: kushuhudia kwamba hakuna wa kuabudiwa isipokuwa Allah, kuwa Muhammad (s.a.a.s) ni mja na Mtume Wake, kuswali, kufunga na kuhiji." (Bukhari and Muslim)*

Ikiwa wakati wa mauti umefika sasa, je! Mtu ambaye hakutekeleza wajibu wake kama mja wa Mwenyezi Mungu ataweza kutoa hesabu ya yote aliyoyafanya akiwa duniani?

Ni nini umefanya hadi sasa ili upate radhi za Mwenyezi Mungu?

Je! Umetekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa ukamilifu?

Huenda mtu akawa na jibu la ndio kwa maswali haya. Lakini akitubu na kufanya jukumu la kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu, ataweza kutarajia msamaha wa Mwenyezi Mungu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.a.s) alikuwa akitafuta msamaha kwa Mwenyezi Mungu mara kwa mara:

*Naapa kwa Mwenyezi Mungu, mimi huomba msamaha na kurejea Kwake zaidi ya mara sabini kila siku. (Bukhari)*

Ni lazima kujikinga na Mwenyezi Mungu, ambaye ni al-Ghaffar (Mwenye kusamehe, Mwingi wa Kusamehe,) al-Halim (Mvumilivu) na al-Tawwab (Mwenye kukubali tauba) kwa hakika Mwenyezi Mungu Atawatuza wenye subira na wanaomrejea. Na kwa hakika Atawasamehe waja Wake ambao wana imani na kuwatuza kwa matendo mema waliyofanya kulingana na uwezo wao. Kwenye Qurani Mwenyezi Mungu anatoa bishara akisema:

**Mlivyo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu (vya jaza yenu) ndivyo vitakavyobakia. Na kwa yakini sisi tutawapa waliosubiri ujira wao kwa yale mazuri waliyokuwa wakiyatenda. Wafanyaji mema, waume na wanawake,hali ya kuwa ni Waislamu, tutawahuisha maisha mema, na tutawapa ujira wao (akhera) mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyatenda. (Surat an-Nahl: 96-97)**

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.a.s) amewahimiza waumini kuwa na msimamo kwa kutenda matendo mema na akawapa bishara kuwa watalipwa na Mwenyezi Mungu wakifanya hivyo.

*Mtume (s.a.a.s) amesema: "Endelea kutenda (mambo mema), kwani kila mtu ataliona rahisi kufanya (lile ambalo litampeleka pahala pake). Kisha akasoma aya " Na Yule anayetoa (zaka, sadaka na vinginevyo) na kumcha Mwenyezi Mungu na kusadiki jambo jema (akalifuata), tutamsahilishia njia ya kwenda Peponi. Na anayefanya ubakhili, asiwe na haja na viumbe wenzake, na akakadhibisha mambo mema, tutamsahilishia njia ya kwenda Motoni."* (Bukhari)

Tusisahau kwamba mmoja wetu anaweza kupatikana na mauti na hata akiwa na majuto, hatakuwa na fursa ya kurekebisha makosa aliyoyafanya. Kwa hivyo tusipoteze fursa ya kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na kufungamana na maamrisho Yake na sunna ya Mtume (s.a.a.s). Hii ndio njia peke ya kuwa mja maybe Mwenyezi Mungu Anamneemeshea rahma na mapenzi. Na ndio njia pekee ya kufika kwenye Pepo, mahala pa kudumu anakotayarisha Mwenyezi Mungu kwa waumini Wake wa dhati.

**Wakasema (Malaika): "Utakatifu ni wako! Hatuna ilimu isipokuwa ile uliyotufundisha ; bila shaka wewe ndiye Mjuzi na ndiye Mwenye hikima. " (Surat al-Baqara: 32)**